



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA BARAZA LA KISWAHILI LA TAIFA (BAKITA)



Baraza la Kiswahili la Taifa [BAKITA] ni taasisi ya Umma chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambayo inasimamia shughuli za ukuzaji wa Kiswahili nchini Tanzania na kuratibu maendeleo yake nchi za nje. Baraza liliundwa kwa sheria ya Bunge Na. 27 ya mwaka 1967 na kufanyiwa marekebisho mwaka 1983 na 2016.

DIRA

Kuwa taasisi kinara ya ukuzaji na uratibu wa Kiswahili duniani.

DHAMIRA


Kukuza na kuimarisha matumizi ya Kiswahili sanifu kwa kushirikiana na wadau.

● Huduma Zinazotolewa na BAKITA


- Kuratibu na kusimamia matumizi Sanifu ya Lugha ya Kiswahili nje na ndani ya nchi.
- Kuhimiza matumizi Fasaha ya Kiswahili katika shughuli za Serikali na za Umma.
- Kushirikiana na vyombo vingine katika kuendeleza Kiswahili.
- Kushirikiana na Mamlaka yanayohusika katika kuanzisha Tafsiri Sanifu ya Istilahi za Kiswahili.
- Kutoa huduma kwa Serikali Mamlaka za Umma na kwa Waandishi binafsi waandikao kuhusu Kiswahili.
- Kushirikiana na Vikundi Taasisi na vyombo mbalimbali vya Taifa kuratibu Utafiti wa Kiswahili unaofanyika katika Jamuhuri ya Muungano.
- Kushirikiana na Wachapishaji kusaidia Waandishi waandike Kiswahili Sanifu.
- Kuanzisha Mashindano ya Uandishi wa Kiswahili.
- Kushirikiana na Wizara inayoshughulikia elimu kuthibitisha Vitabu vya Kiada vilivyoandikwa kwa Kiswahili kabla ya kuchapishwa.
- Tunatoa huduma ya Tafsiri na Ukalimani katika Lugha za Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kichina, Kiarabu, Kireno, Kirusi, Kijapani, Kihispaniola n.k.
- Kutoa mafunzo ya Kiswahili kwa wageni wanaotoka mataifa mbalimbali kwa ufanisi mkubwa na gharama nafuu.
- Tunatoa mafunzo ya Kuimarisha Stadi za Kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa walimu wenye shahada za Kiswahili.

+255 774 399 975


km@bakita.go.tz



bakita_tz



bakitatz



Bakita TV